



UN-HABITAT

**UJUMBE WA MKURUGENZI MTENDAJI
SHIRIKA LA MAKAZI DUNIANI
SIKU YA MAKAZI DUNIANI
4 OKTOBA 2004**

Umoja wa Mataifa ulichagua siku ya Jumatatu ya kwanza ya mwezi Oktoba kila mwaka kuwa Siku ya Makazi Duniani (SMD). Ni tukio linaloeleza hali halisi ya makazi na haki ya msingi ya kupata makazi bora kwa wote.

Kauli-mbiu ya Siku ya Makazi Duniani hapo tarehe 4 Oktoba mwaka huu ni, “Miji-kama kiini cha Maendeleo Vijijini”. Tulichagua mada hii ili kuonyesha utegemezi uliopo baina ya masuala ya kiuchumi, ya kijamii na mazingira kati ya miji na vijiji. Maendeleo endelevu yanaweza kufikiwa pale tu tutakapoangalia maeneo haya kwa umoja wake, kama sehemu zinazotegemeana.

Mahusiano baina ya miji na vijiji yanategemea sana miundo-mbinu inayoyaunganisha. Mahusiano haya huboresha mtandao wa miundo-mbinu, uzalishaji huongezeka, huboresha soko la wakulima vijijini, hutoa taarifa mbali mbali na ajira. Miji husimama kama mvuto wa biashara toka vijijini, na lango la soko la biashara ya kitaifa na kimataifa. Wanafaidika kutokana na mazao ya wakulima toka vijijini.

Pakiwepo kiungo muhimu kati ya miji na vijiji, ndivyo pia itakavyokuwa rahisi kwa wakazi wa vijijini kupata kazi mijini, na matokeo yake ni kupunguza matatizo ya ajira vijijini. Ni muhimu kwa miji kutoa ajira kwa nguvu-kazi ya ziada iliyoko vijijini. Katika nchi zinazoendelea, maendeleo hafifu mijini yamekuwa ni kizuizi katika kutafuta njia mbadala ambazo vinginevyo zingekuwa wazi kwa ajili ya watu vijijini.

Tatizo linalohitaji ufumbuzi katika nchi zinazoendelea ni ukweli kuwa miji midogo na ya kati inapata mgao kidogo na haiendelezwi. Hali hii inaweza kurekebishwa kwa kuboresha barabara, reli na kuimarisha mtandao wa mawasiliano muhimu kati yake. Maendeleo ya kiuchumi katika miji midogo ni ya manufaa katika shughuli za kiuchumi vijijini kwa sababu ya mahitaji makubwa ya mazao toka huko kwa ajili ya wakazi wa mijini amabao pia wana uwezo mkubwa wa kununua mali hizo.

Miji ya karibu huwa ni sehemu ya kufikia wahamiaji toka vijijini ili kutafuta maisha. Pia kupunguza madhara ya wahamiaji walio wengi waendao mijini.

Katika nchi nyingi maskini, hali halisi ya makazi vijijini ni kuwa mbali mbali, na hii husababisha hutoaji miundo-mbinu (infrastructure) na huduma nyingine muhimu kuwa ghali sana. Ni wazi kuwa sababu za kutoendelea kwa vijiji vingi ni kutokana na kuwa na miundo-mbinu dhaifu na huduma hafifu kama vile barabara, mawasiliano, huduma za

afya, elimu, mikopo, masoko na upashanaji habari. Vitu hivi vinaweza kutolewa na kusimamiwa na idadi ya wakazi wengi waishio mijini.

Kwa hiyo basi ni muhimu kutambua kuwa, kama tutapenda kupata maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii kama taifa, serikali zetu zitalazimika kuunganisha maeneo ya miji na vijiji kama sera ya nchi. Kichocheo cha maendeleo sawia kati ya miji na vijiji kama majimbo ni kuimarisha vyombo vya mipango katika ngazi ya taifa, mkoa na wilaya.

Katika siku hii ya makazi duniani, tunatoa wito kwa wadau wote katika maendeleo vijijini, kuunganisha maendeleo mijini katika mipango yao ili kuleta mkabala wa jumla kwa ajili ya maisha yetu wote: Miji yaweza kuwa kiini cha maendeleo vijijini.